

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, YATTA CONSTITUENCY, HELD AT
MATUU CATHOLIC CHURCH HALL**

ON

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, YATTA CONSTITUENCY, HELD AT MATUU CATHOLIC CHURCH HALL ON 21ST MAY, 2002.

Present:

1. Com. Phoebe Asiyo
2. Com. Mutakha Kangu
3. Com. Charles Maranga
4. Com. Pastor Zablon Ayonga

Secretariat Staff in Attendance:

1. Peter Kanyi – Programme Officer
2. Lydia Manyoni – Assistant Programme Officer
3. Jacqueline Nyumoo – Verbatim Recorder

The meeting was called to order at 10.00 a.m with Com. Phoebe Asiyo in chair.

Rose Kimeu: Sasa tungependa kuanzisha mkutano wetu wa leo. Kama ilivyo desturi yetu sisi huanza kwa maombi. Na nitamuuliza mmoja wetu mwenye ataongoza aweze kutuomba tuanze mkutano wetu wa leo. Tafadhali tuombeni.

Speaker: Ee baba Mwenyezi Mungu Mtakatifu uliye juu Mbinguni, Muumba Mbingu na vyote vijazavyo ulimwengu huu vilifanyika kwa uwezo wako, tunajua kabla yako na mbele zako hakutakuwa na mwingine kama wewe. Hakika Mwenyezi Mungu tunanyenyekea mbele zako, tukilisujudu na kulihimidi jina lako lililo takatifu, na ambalo lafaa kuinuliwa katika kila hali. Tumekusanyika mahali hapa tukiwa na lengo moja na kusudi ambalo ni kutoa maoni, ili kila moja ashiriki kwa ajili ya kuwa na maendeleo yanayostahili. Hasa kwa sababu ya kujenga ulimwengu huu na nchi yetu kwa ajili ya utukufu wako. Hebu Jehova utupatie wakati mwema tunaposhiriki mahali hapa tukaweze kuyaelekeza macho yetu katika siku za usoni kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Walio mbele zetu Mwenyezi Mungu ukaweze kuwapatia hekima ili tukaone wakati ulio bora siku ya leo. Bariki walio njiani ili tukaweze kujumuika nao, na kuona tumekamilisha jambo hili kwa wakati unaofaa. Hayo yote ninaomba nikiamini yatawezekama kupitia kwa jina safi la mwanao Yesu, Amen.

Rose Kimeu: Asante sana. Ijapokuwa jana tulifanya introduction ya wale members wa Constituency Committee, leo nitaweza kuwa-introduce tena kwa manufaa ya members of public wenye wako hapa. Kwa hivyo nitaita wale members of the Constituency, Constitution Committee mukaweze kusimama tuwajulishe. Karibu na mimi hapa kunaye Elizabeth Mokola, Elizabeth ndiye Secretary ama Katibu wa ile Committee. Mbele yake kuna Mr. John Kemuya, who is the Chairman of the

Constitution Committee. Pale kuna Mr Joseph Mukunzu ambaye pia ni member. Mbele ya Mukunzu niko na Pauline Chonda, aliye pia member wa Constituency Committee. Anayeingia sasa ni Augustine Manyi, ambaye pia ni member wa ile Kamati. Kwa hivyo hawa ndio members wa ile Kamati yenye imeshughulikia marekebisho ya Katiba katika eneo hili la ubunge. Mimi ninaitwa Rose Ngina Kemeu, mimi ni District Coordinator wa Constitution of Kenya Review Commission, Machakos. Asanteni. Kwa upande ule mwingine tuko na wale Secretariat Members wenye wametoka Nairobi na pia tuko nao Commissioners ambao wamekuja leo kusikiza maoni yetu. Wao watajitambulisha kwenu. Asanteni.

Com. Phoebe Asiyu: Asante sana District Coordinator wetu kwa kuwajulisha wale walio hudhuria Kamati hii ya leo ya kuongea mambo ya Katiba kwa wale ambao wametusaia sana kuongoza mwendo huu tangu ulipoanzishwa. Pale kando upande wangu wa kushoto ni wale waliokuja nasi kusaidia kusikiliza na kuandika kila kitu kwa mkono na pia kwa machine ili tusije tukasahau wakati wa kujadiliana na kuandika Katiba mpya mambo yale ambayo yatatolewa hapa leo. Hapa juu tuko maCommissioners wa Commission. Upande huu ni Mr. Mutakha Kangu, ambaye ni advocate of of the High Court na pia ni mkufunzi katika University ya Moi kule Eldoret. Upande wangu wa kushoto ni Pastor Zablon Ayonga ambaye pia ni Mwana Kamati wa hii Commission. Mimi ni mama Phoebe Asiyu, pia Commissioner wa kutayarisha Katiba mpya ya Kenya. Tumeshukuru sana nyinyi kufika hapa. Ningependa kuwapatia maCommissioner wenzangu nafasi ya kuwasalimia kabla hatujaanza mkutano.

Com. Pastor Ayonga: Hamjambo?

Audience: Hatujambo.

Com. Pastor Ayonga: Karibu sana

Commissioner: Nawasalimu, hamjambo.

Audience: Hatujambo.

Commissioner: Nawashukuru mumekuja, na tunafikiria tutashinda na nyinyi kwa njia sawa. Asanteni.

Com. Phoebe Asiyu: Asante. Nitakuwa Mwenyekiti wa hiki kikao kwa muda mchana huu wa leo. Tuna mpango wa vile tutaendesha kikao hiki hapa Matuu. Wale ambao wamejiandikisha majina hapa ni watu kumi, na tutaanza kuwasikisa kwa maana tunatumaini watu wengi sana wa matuu watakuja kutoa maoni yao. Vile mnavyojua, sisi kama Commission hatuko na maoni yetu, na hatutaandika maoni yetu. Yale ambayo nyinyi mtatueleza ndiyo tutachunga na tutaandika na italinganishwa na maoni ya watu wote wa Kenya. Kwa hivyo ni kazi ngumu sana. Tutaweka sauti ya kila mtu kwa mashini, tutaandika kila kitu verbatim vile inafanywa kwa Bunge, na sisi wenyewe tutachukua notes zetu yale mambo ya maana ambayo ni lazima tujadilie na tuandike ili Katiba ya Kenya ionyeshe mahitaji ya wanaKenya.

Nitoe historia fupi ya Katiba hii: mnajua watu wa Kenya kwa miaka kumi wametaka sana kupata Katiba mpya. Bahati nzuri watu wa Ufungamano na wa Parliament walisikilizana wakaweka Commission moja ambayo sasa inazunguka Kenya nzima kutafuta maoni ya watu. Tuliwatumia fikira zingine ili mpate kusoma juu ya maKatiba za nchi zingine na nchi hii, na mahitaji ya watu wa Kenya vile wamekuwa wakizungumza tangu miaka kumi iliyopita. Mambo yalio kwa hicho kitabu chekundu na maswali siyo mwisho wa fikira zenu. Hiyo ni kuwaongoza tu vile mtafikiria, lakini tunajua mnaweza kuwa na maoni na hekima ilio hata tofauti na yale ambayo sisi tuliwaletea kama muongozo ili muanze kufikiria mambo ya Katiba mpya. Kwa maoni yetu tunataka tumalize Katiba hii haraka, na hatungependa kufanywe election kabla hatujakuwa na Katiba mpya. Kwa maana tunaona vikwazo ambazo zitakuwa hapo mbele maana watu wamekuwa na hitaji kubwa sana ya kuwa na Katiba Mpya na watasikia uchungu sana kwa mioyo yao wakiambiwa watafanya uchaguzi tena mwaka huu bila kuwa na Katiba mpya. Jana tuliko mpaka karibu usiku. Katangi kule ambako tulikuwa jana. Leo pia tutakaa mpaka tutasikiliza mtu wa mwisho kama watu watakubali kuja, ili tuweze kuweka mambo pamoja na tufanye kwa haraka iwezekanavyo. Pia vile mnajua tulichukua miezi tisa kabla hatujaanza kazi hii, tuingojea masikilizano yaweko katikati ya Bunge na Ufungamano. Imekuwa kazi ngumu lakini tumejaribu na tunaona kama tutashinda. Tunataka maoni yenu yawe sawa sawa ili itusaidie kufanya kazi kwa haraka. Nyinyi pia mufahamu ile shida ambayo Commission hii iko nayo. Mnajua this is a very highly political process, na ni wananchi tu watasaidia. Tunajua nyinyi muko pamoja na sisi, mtatusaidia kuweka Katiba mpya kabla ya uchaguzi ujao. Kama itakuwa ni lazima iongezwe siku mwezi moja miezi mbili haitauwa waKenya lakini heri uchaguzi ifanywe kwa Katiba mpya. Hiyo ni fikira yetu sisi.

Kwa sasa niko na hawa watu ambao wako tayari kuongea ni maBwana Simon Ntaya na Paul Mkulima, Joseph Katiko, Muli Ntolu, Ruth Betty, Gladys Kinyanjui, Daniel Mutisia, Tabitha Mathews, Patrick Nzioka na Elisabeth Muasha. Bwana Simon tafadhali ukiwa tayari uje ukae hapa, tutakupatia mashini uonge kutoka hapo.

Simon Ntaya: Labda tuna njia fulani, ambayo tutatumia kuyajubu maswali ama tu ni vile nimekuja nimejitayarisha? Lazima nifuate muongozo ama nikiholela holela tu?

Com. Phoebe Asiyo: Vile tutafanya, utakuja hapa, na wewe ni Bwana Simon? Kuja tu ukae hapo, halafu kama una swali ambalo linakusumbua kabla hujaongea utatueleza. Lakini kama una kitu umeandika tayari na utatuachia, hiyo itakuwa mali yetu, ukitoka hapa utatuachia. Kwa hivyo utapata dakika tano za kutaja tu mambo yale ya muhimu kutoka kwa hiyo karatasi yako, karatasi tutabaki nayo tutaweka kwa computer yetu. Kama haujaandika, pia tutakusikiliza oral na tataandika kile kitu ambacho unasema.

Nilisema hapo mbele hiyo mambo ya maswali na issues zile tulileta ilikuwa ni ya kuwasaidia tu, tafadhali usifuatane na hiyo. Wewe sema ile mambo inatoka kwa roho ambayo ina inakuhusu, juu ya serikali, ile system ya serikali ambayo ingefaa watu wa Kenya, juu ya mambo tumesema kwa separation of powers, juu ya mahitaji ya wananchi, juu ya political parties, lakini iwe ni

fikira yako tu siyo fikira ya hiyo kitabu. Asante.

Com. Pastor Ayonga: Isije iwe kana kwamba kile kitabu mlio tumiwa ni text book, na leo ni siku ya kujibu maswali ya hicho kitabu. Sisi hatukuja kujibiwa hiyo, kwa maana tunajua majibu ya hiyo. Tumekuja mtupe maoni yenu, usije ukatuendesha useme swali number one, muliuliza hivi na hivi na hivi, jibu ni hii. Hatutaki hayo, tunataka maoni yenu. Munataka Kenya ya namna gani? Katiba ya namna gani? Tumeelewana? Kwa hivyo musahau kile kitabu for now, tuambie maoni. Hatukuja hapa ili mutuulize maswali. Leo hatukuja hapa tuulizwe swali tujibu, leo ni wewe unayetupa maoni jinzi unavyo fikiria. Maoni yako tutayaheshimu jinsi ambavyo unayatoa.

Com. Phoebe Asiyu: Utakumbuka kwamba hapa tulipo, mahitaji ya nchi hii ni tofauti na mahitaji ya Central au ya Coast au ya Nyanza au Western. Kuna mambo fulani ambayo pengine kama maji, wale wanakaa Lake Victoria hawana shida ya maji, si ndio hivyo? Kwa hivyo yale mahitaji ya upande huu tukijua ni vizuri zaidi, pamoja na yale ambayo mutaongea juu ya Katiba mpya. Asante.

Simon Ntaya: Yangu Bwana Mwenyekiti Madam Mwenyekiti,

Interjection. Com. Phoebe Asiyu: Utasema jina lako.

Simon Ntaya: Jina ni Simon Ntaya, Simon Ntaya nimetoka Ndalani. Madam Mwenyekiti mimi nitatoa maoni juu ya role of the armed forces. Wanajeshi wetu, namaanisha Kenya Army, Air Force na Navy, raia hatuelewi waajibu wao katika utekelezaji wa maendeleo ya nchi yetu. Ningaliomba Katiba yetu mpya wawe karibu nasi, wasiwe ni watu kama wanatoka mwezini, tunawaona tu wakati wa sherehe na wa parades. Kwa mfano, nchi zingine huwa majeshi yao inasaidia tuseme paa la shule limetolewa na upepo. Hapa sisi kama raia tunaona wakifanya kazi. Tunasikia kuna engineers battalions wanafanya drilling of bore holes, lakini hatujawahi kuona wakituzaidia. Huku kwetu Yatta shida ya maji imezidi, tumejaribu kama vikundi kupata contractor na tunaelewa kwamba wanafanya lakini hatuelewi kazi yao ni gani. Tungeomba ishirikishwe katika Katiba yetu.

Wanajeshi wanapokosea huadhibiwa. Kuna court marshals, na hiyo court marshals ni siri hivi kwamba hata raia wengi hawajui kitu marshals kwa kiKamba ni kitu gani. Hatukatai ni siri yao, lakini huwa inakuwa abused, ili kwamba wakikosea kwa sababu hakuna press mambo yao ni mwisho. Yule askari anaumia bure.

Kingine ni radio communication kwa police, mara nyingi tumesikia police wanatumia one channel; wale wa traffic wale wa nini. Nikifungua radio nikiwa kwangu nyumbani naweza kunasa mazungumzo ya polisi wakifukuza wezi. Police wawe na channels tofauti, kwa mfano wale wanekimbiza wezi wasiwe wanasikizwa na wale wengine wako barabarani.

Kuna shida nyingine imekuwa kwa Katiba yetu hasa Education Act. Education Act ilioko ni ya wakati wa zamani serikali

ilipokuwa inatoa grants, siku hizi ni wazazi, kwa ile cost-sharing. Tumekuwa na PTA ambayo haiko kwa vitabu, PTA ambayo ni toothless bull-dog, na hawa ndiyo wenye kutoa pesa. Kwa hivyo Katiba mpya tunaomba wazazi na pia PTA washirikishwe. Iwe kwamba the whole of the Education Act iwe over hauled kwa sababu ukiitazama vizuri, ni ya wakati serikali ilikuwa inatoa pesa. Kumekuwa na mwomngozo fulani kwa mfano, ambapo unakuta kama Ministry of Education, mambo ya tendering boards/committees mwongozo ni wa Ministry of Finance. Wazazi ndio wanatoa, wanakuwa dictated to na mtu ambaye hatoi. Asante.

Com. Pastor Ayonga: Bwana Simon sikuelewa ulitaka aje katika hii court marshals ungependelea nini?

Simon Ntaya: Ningalipendelea kuwe na namna ya ku-counter...

Interjection. Com. Pastor Ayonga: Sema kwa Kingereza kama expression inaweza toka vizuri.

Simon Ntaya: Tuwe na jinsi ya, hatitaki raia ati waende huko wakasikize, iwe ni open court. Lakini tuwe na mechanism ambayo tunaweza counter any under-dealings.

Com. Phoebe Asiyu: Okay, mimi ningependa kujua umeleta fikira tofauti kabisa. Ningependa ufafanue zaidi juu ya kazi ya Armed Forces, you are saying that we don't know them, that in fact we don't even know what they are doing because we are not at war with anybody, and they are there getting salaries. You want them involved in the development of this nation. Because as you have said wako na maingeneers, na wana machinery na wamaweza kuchimba dams. Tafadhali ningependa ufafanue zaidi kazi ambayo unafikiria watu wa Armed Forces wakifanya, nchi hii ya Kenya inaweza kupata development haraka zaidi.

Simon Ntaya: Nilikuwa, Asante Madam. Nimetoa mifano miwili ya kwamba wengi hawajui kwamba kuchimba visima vya maji, wako na machine za kisasa hata tunapozungumza. Tungeomba kwa sababu ziko na hutumika na wachache walio na uwezo, niseme ni politically connected, nitasema hivo kwa sababu hivo ndiyo trend ilioko. Kama ni shule ama kanisa ama kikundi chochote kile, mukiwaandikia watajibu kwanza mupitie Department of Defence na itachukua miaka kumi hata labda hautajibiwa. Kwa sababau wako na mashine, watumie njia inayofaa. Wasiingiliwe na siasa, wahudumie raia. Kama ni shule imeng'olewa mabati na upepo, hiyo kazi wanaweza kusaidia. Nchi zingine kama India wako na kile wanaita National Cadet Course. Utakuta kwamba wao hata wanatangaza kwa bill boards, for an exiting career join the Kenya Air Force. Juzi liniona wamejaribu, lakini hapo zamani haikuwa hivo. Ndio watoto wetu wakienda jeshi, huwa hawaelewi ni kitu gani, wanaenda kufanya nini. Huwa wanafikiria tu askari ni kupigana. Umeuliza kama hakuna vita watakuwa wakifanya nini. Hiyo miradi kama kujenga bridges, walifanya kazi nzuri kule Mombasa, lakini wakati mwingine tunaona ni kama siri hatuelewi na wako na kila kitu. Hiyo,

Commissioner: Unatuambia, badala tuweke watu kwa Armerd Forces kuka bure, na sana sana wanachukua wale watu wa

nguvu kabisa, When they have identified, they look for tough men and women, badala ya kuwaweka wakae bure huko, we should find a way of involving them in the building of the economy, that is what you are telling us?

Simon Ntaya: Partly

Com. Phoebe Asiyo: Ya pili ni kwamba there has been this tendency of our people, unajua wanangoja war which might never come because you people are always in churches praying that we should not have war and God hears us any way, they don't do anything. These days kitu tunasikia wameenda "peace-keeping". Swala nataka kukuuliza hapo hii "peace-keeping" wakienda, they go to vey many countries. They only earn personal allowances. Can we start thinking as a country of asking for some payment, we cannot just be "keeping-peace" for nothing? Or what do you say?

Simon Ntaya: Correct, na kabla sijajibu swali lako nilikuwa nikisema utaona kwamba tunaelezwa kwamba Kenyans tuko na tabia ya ku-react and we are supposed to be pro active. Tunangojea tu maneno itendeke ndio tuanze kurakaruka. Hiyo peace-keeping troops kama askari wetu hawa, national disasters, tukiwa na strategies ya ku-focus na tuko na hawa askari wetu, wako kutusaidia kwa hizo. Vile wanavyoenda nje kama ni peace-keeping troops, na ni sisi tumetoa vile amesema wanapatiwa mishahara yao which is idea ya kibinafsi. Kama nchi hatufaidiki. Sisi ndio tumewafanyia training, kila kitu ni pesa yetu ya raia, ni kodi yetu, lakini wanaporudi hatuna faida. Hata wakirudi wana resign hawatufanyi kazi. Unasikia fulani ako na ujuzu, ameenda Sierra Leon, ameenda wapi na wapi, lakini huo ujuzi wao hatutumii, hata faida wanazopata huko hatusipati. We want them to plough back.

Com..... At the international level, we should negotiate.

Simon Ntaya: Correct.

Com..... That negotiating with the UN that we have given free services for far too long, now we want to be paid.

Simon Ntaya: Correct.

Com..... Well thank you, maybe I have one question, are you happy with the kind of the Armed Forces we have, you want it increased or decreased, have you ever thought about that?

Simon Ntaya: It is to big for no apparent reason I should say. Kuna jambo la madaraka kama Generals wetu. Wakati mmoja nilikuwa mahali na yule mwalimu alikuwa ni rika moja na Mulinge alipokuwa Chief of General Staff Kenya. Yeye alikuwa ni Major Promotions mean money, hata kwa head teachers. Huwezi kuwa in one school na three Headmasters or Principals. The Generals are too many, over-taxing the tax fair. They are too many, the establishments are harphazardly done. Labda

nimekujibu. The strength of the force should determine the number of Generals. Wakati mwingine unakuta a floating General, ni kama reliever in a martanety case. Have I answered you?

Com..... Yes what I was thinking the actual numbers.

Simon Ntaya: Is too big for no apparent reason.

Com..... Okay

Simon Ntaya: Thank you.

Com.Phoebe Asiyo: Sasa tafadhali uweke register yetu jina lako ili ukipata mambo ulisema haikuandikwa sawa sawa, tunaweza kukutafuta tukupate na wewe pia uje utuambie mambo yangu haikuandikwa vizuri. Ningependa kumuuliza Bwana Pauline Mkulima ambaye ni business-man hapa Matuu aje aongee na sisi. Tafadhali ukianza useme jina lako unaswe na hii mashini halafu uanze kuongea.

Paul Mkulima: Kwanza nashukuru kabisa kwa nafasi ambayo nimepewa. Nawashukuri maCommissioner kwa kupata nafasi ya kutembelela upande hii ya Yata. Jina langu naitwa Paul Moya, au kwa jina lingine Mkulima. Mimi ni mfanyi biashara hapa Matuu, na mimi ndio Mwenyekiti wa chama cha National Party of Kenya NPK, hapa Yata na Katangi division mbili.

Bila kupoteza wakati nitaenda moja kwa moja, niseme ambayo nilikuwa nimetayarisha ili nao wengine wapate nafasi ya kuja hapa na kesema yao. Kwanza kabisa ni maoni yangu uchaguzi wa hapa Kenya uchukue miaka minne na siyo mitano. Kwa sababu miaka mitano ni mingi zaidi. Kama uongozi hi mbaya watu wanasumbuka wakiangalia miaka mitano itakwisha lini. Kwa hivyo kama miaka ingekuwa minne badala ya mitano ni maoni yangu hiyo ingekuwa sawa. That includes Presidential, elementary and civic.

Ni maoni yangu ya kwamba there should be an impeachment of a President who doesn't deliver that in Kenya. Kama miaka mitano hijakwisha na rais ambaye amechaguliwa hajafanya kazi vizuri kupigwe kura ya maoni, referendum ya kumuondoa na iwe katika Katiba. If there is a referendum na watu wanaonelea maoni yao yote huyu rais hawapeleki vizuri, aondolewe, lakini kupitia kwa kura ya maoni ndio nchi ikaweze kuwa na amani. I am suggesting notice to referendum of about six months and them we go to it.

I am suggesting if an MP is elected to lead the country kama rais/President, yule ambaye alikuwa namba mbili au runner up, kule alikuwa anagombea kiti, awe ndiye mjumbe wa sehemu hiyo. Kwa sababu tumeonelea rais hawezi kutimiza mahitaji ya watu wa sehemu yake kwa sababu anaangalia nchi yote kwa uzima, na anakwenda mbali nchi za inje, akijaribu kuomba pesa ya kuzaidia nchi na mambo mengine kama hayo. Kwa hivyo ningependelea kuwe na mjumbe hapo rais ametoka, yule jama

alikuwa namba mbili aende Bungeni kama mjumbe.

Naonelea Mjumbe akichaguliwa mchache hafanyi kazi vizuri na kuna malalamiko ya Constituency mengi, baada ya miaka miwili, pia kuwe na referendum katika Constituency level. Kama hiyo haiwezekani, wananchi wenyewe wa sehemu hiyo wampeleke kotini waeleze maelezo yao huko ni kwa nini wameonelea hawasaidiki kutokana na services za Mjumbe wao. That is within the next two years, lakini ikipita hapo mwaka wa tatu, aachwe amalize wakati wake.

Mimi naonelea Mayors na Chairman wachaguliwe na raia. Hayo yamekuwa maoni ya watu wengi lakini inafaa ikitoka mdomoni mwangu, kwa sababu Waswahili wanasema “walio wengi wape, ukiwanyima, watajinyakulia kwa wingi wa mikono yao”. Kwa hivyo mimi nasema kama hawa wengine Mayors na Chairmen wachaguliwe na raia, ndio County Councils ziendeshe vyema.

President, MPs, Concilors, Chairman and Directors of Parastatals must have a stable family. Kama mtu ni Mjumbe, ni Councillor, President, lazima awe na bibi au na bwana. Kama mtu hana bibi au bwana asichaguliwe kwa kiti chochote kwa sababu uongozi unatoka nyumbani. Natumai nchi ya Kenya wengi ni Wakristo na kuna Waislamu. Na kama wewe ni Mkristo au Muislamu, unajua maandiko ya kitabu chenu yanaweka nguvu hayo.

Kama kiongozi ako na mabibi wawili ameshawahi kuowa tayari mimi ni maoni yangu kusikubaliwe afanye harusi na bibi mmoja. Afanye na hawa mabibi wawili tayari, kwa sababu asha waowa. Hata kama atafanya na moja huyu mwingine awe hapo pembeni n apewe cheti chake cha marriage. Kwasababu watu wengi wametumia marriage certificate kusumbua watu sana. Mtu anafanya harasi na bibi mmoja anaowa wengine watano na sheria nayo inaangalia cheti cha harusi. Hiangali hawa wengine, and the Christian Marriage Act says, that if you have wedded only one person, hawa wengine wote are not recognized by law. Kwa hivyo ni maoni yangu at least mtu apatiwe marriage certificate ya mabibi maximum wawili kama ashawahi kuowa tayari.

Kama mtu ni kiongozi kama President au Waziri, in every official function, awe accompanied by the wife. It has been rumoured here in Kenya that the Ministers cannot go to public functions with their wives because of, I don't know what but there must be a reason. Maybe it looks like they are embarrassing somebody. We don't want that, that is why we are saying a leader should have a stable family,

Com. Phoebe Asiyu: Why don't you just talk and finish now...

Paul Mkulima: Yes I am saying kama hapa Kenya, inasemekama waziri akienda katika state function na bibi yake ataaibisha rais, kwa sababu rais hana bibi. Mimi nimesema sasa nikitokea vile ulisema nikitumaini sitashikwa nikitika hapa hivi.

Com. Phoebe Asiyu: Huku (inaudible)-----vikao vyetu hakuna mtu anashikwa.

Paul Mkulima: Basi umesema nitoke kabisa niwache kujifungiafungia pale. Kwa hivyo hapa Kenya ndio unaona hakuna Waziri anaweza kwenda ka state function akiwa na bibi yake kwa sababu nilisikia waliambiwa yule anakuja na wake anataka kuembarass the President who may- be he doesn't have one or something like that. Kwa hivyo iwe ni sheria wakitokea, wanatokea na mabibi zao ndio waonyeshe young generation a good example.

And if a public leader is divorced he should cease holding public office,

Com. Phoebe Asiyu: If?

Paul Mkulima: If a public leader is divorced, he should cease heading a public office. I think that is prominent in America although we are not trying to copy the Americans. If you divorce, you are no longer a minister, you are no longer a congressman, you are no longer in Parliament, you are no longer holding any public office. Ukisukuma bibi yako akwende kwao, na wewe kile cheo chako unacho kinakwenda mara moja.

I am insisting there should be medical examination for public leaders. President, Members of Parliament, Councillors wafanyiwe uchunguzi wa kiafya and particularly terminal diseases, yale magonjwa hayana dawa ndio tuweze kusaidia uchumi wa Kenya and avoid going for a by- election because it is very expensive. Kama rais au mjumbe anafanyiwa medical examination na anapatikana he is not fit especially, and I mean especially terminal diseases, akipatikana yuko healthy, then let him forge ahead.

I am insisting also even in future, people like, kama nyinyi watu wa Katiba sasa mnachukua maoni yetu, hata nyinyi lazima uwe na good background even from the family. Kwa sababu hutachukua maoni ya mtu mwingine ukiwa huna back-ground nzuri kutoka hapo kwako nyumbani, ofisini na kwa kijiji chako. Uwe na recordi nzuri. Okay

Com. Interjection: (inaudible)-----

Paul Mkulima: Okay, I did not talk about medical examination for you because yours is shortlived it can take a year or so. But I am talking about a public leader who is taking about four, five years in the office. Yours is about a year or less that was my point.

I am insisting Presidential aspirants should be given TV public contest like we have in America, waeleze wananchi wanataka hiki kitu kwa nini kupitia kwa runinga. Kama ilivyo Germany, England and America. Kama kuna channel ya serikali, ikubaliwe kutumika na kila mtu hata kama ni wa upinzani. We do not want an atmosphere like the one we have in Kenya, you only hear the opposition in KBC when they are fighting, when they have done good things they don't appear any-where. That is a thing we want rectified in our Constitution.

Com. Phoebe Asiyo: Time is running, let's...

Paul Mkulima: I am just, give me two minutes I will finish up. I am just mentioning, I am insisting the President, MPs, Councillors and what have you, must have minimum education of form four, and pass for that matter.

The powers of the President must be reduced to appoint parastatal heads, forces heads, administration, security, and what have you.

Any leader who is found to practice nepotism and tribalism by virtue of his position should be taken to court, and there should be a channel of reporting this leader to the public.

There should be an allowance to criticise the court proceedings without being taken to court na kushitakiwa kwa contempt of court. The courts look to be super-naturally so high nobody can talk about them, ni kwa sababu wanaogopa kushtakiwa, kwa contempt of court, and they have misused that.

There should be Presidential elections alone and parliamentary together with civic in a different stage. All of them ziachane na miezi sita.

There should be no burial to day kama hakuna maelezo ya huyu tunayezika ameuawa na nini, kwa sababu hiyo imesababisha Ukimwi ukose kuisha. Kutaja huyu tunayezika ameuawa na Ukimwi, inakuwa ni taboo, ni makosa, lakini ikiwa ni lazima kutajwe, yule ambaye ameachwa na huyo hakuna watu wataenda kuchukua Ukimwi kwake, na maafa yatapunguka. Kama itakuwa ni lazima administration itaje the cause of the death as one of the most important things to be mentioned in funerals.

There should be Divisional Orphans Fund for the AIDS victims: Kuna watoto wengi wameachwa na wazazi ambao wamekufa kwa Ukimwi. Tukiweka fund kwa constituency level ya kuwazaidia itakuwa ni vizuri. I am finishing just let me say the last one as I finish. Give me two minutes sorry, sorry for that.

Com. Phoebe Asiyo: No, no, no not two minutes just half a minute.

Paul mkulima: Half a minute kwa sababu utaniuliza maswali. I am insisting the Police, the Prison and all that should have their union ya kuwapigania kwa sababu wananyanyaswa sana, kuna ukabila mwingi katika Kenya Army, Kenya Police, na hakuna hata mmoja anasimama kuongea kwa sababu hawana chama chao cha kuwatetea. Jeshi na Police imejaa ukabila, kuandikwa huko ni ukabila, promotion ni ukabila. Kwa hivyo I am insisting there should be a trade union covering the forces. Sorry.

Com. Phoebe Asiyo: Asante sana kwa maoni yako, sasa tuta.....

Com. Now Bwana Mkulima I have some questions for you. You are saying that if an MP is elected President, the second best candidate in the Constituency should become the MP. Our experience shows that in most cases those who become Presidents are never opposed in their constituencies, who will take over in such circumstances? Number two, you are saying that leaders should be allowed to celebrate marriages with a maximum of two wives. Our experience shows that Muslims allow up to four wives. What are we going to do about that?

Com. Phoebe Asiyo: Before you respond, there is a question that I wanted to put to you which is connected to...

Com... Three, you are saying that leaders must be accompanied to all public functions by their spouses. If my wife has her own profession and we know our public functions are too many, is she going to stop her job, and are you going to put her on salary as a wife of a leader or what are you going to do? And finally, you are saying that leaders who divorce should cease having those offices. We know that one of the most respected African leaders Nelson Mandela divorced his wife, while he was still President, in fact he attended court proceedings and gave evidence, and the whole world is so happy that is one of the best leaders Africa has ever produced. I will tell you that in fact what Mandela did in South Africa is a reflection of that society. Very many people you meet are either in their second or third marriages after they have divorced several times. The America you have referred to very many people are in their fifth, seventh marriages after they have divorced several times. What is so special about this, because you will lose your leadership position...

Com. Phoebe Asiyo: There is a question that is connected one of which he is asking and I want you to answer it at the same time. On the election of President leaving the seat for the next most popular person. You are representing the national party of Kenya?

Paul Mkulima. Yes

Com. Phoebe Asiyo: If today you are elected or your party leader was elected, the MP for the area, and also the President and the next most popular candidate was a Kanu candidate, would you still prefer that the National Party of Kenya President accepts the Kanu candidate in the area, although most of the voters in that area are members of the National Party of Kenya? Number two, you are talking about all leaders must have stable families,

Paul Mkulima: Sorry let me have a biro to write my points

Com. Phoebe Asiyo: You can take mine because we need your help. You are saying that every leader must have a stable family and must have a wife that accompany them everywhere, or a wife who is accompanied by the husband. Now where a wife dies and the man does not want to have another wife or where there is a divorce like in the case of Mandela or even where

a husband dies like in the case of Nyiva Mwendwa, are you telling us that these people cannot lead this nation, that they cannot even participate in the leadership of their own constituencies or even their County Council? Thank you.

Com.... There are still many more.

Paul Mkulima: Yes, no problem, I will respond.

Com. Phoebe Asiyo: You can respond to those two.

Paul Mkulima: I can even respond to the others, there is no problem.

Interjection. Com. Then we will give you the other part.

Paul Mkulima: Okay, let me talk about a case involving Nelson Mandela. I would say we cannot use Mandela as a mirror for the whole of Africa because Mandela is one person as such. Secondly Mandela is a person we were giving sympathy support having been jailed for so long. So, much of our support to Mandela was sympathetic (inaudible)----- as such, if I may say so.

Com..... Neither can we use Moi as the example for Africa because we don't know

Paul Mkulima: Well,

Com. Phoebe Asiyo: In any case let us give a bit of sympathy to Mandela's wife, she is still very powerful in that country.

Paul Mkulima: That is very true, that is very true. What I was saying, my dear brother, is generally. Now we are quoting Moi and Mandela, but I was talking generally, I am not so much on the Moi issue, neither on the Mandela issue because I have said we were giving Mandela sympathetic support for having been jailed for so long. Okay on the other side of Kenya, I am not talking so much about Moi, I just imagined. It is my view, if somebody is widowed, that is a different case. There are so many people who when they go to parliament, they divorce because they want to get dot-com ladies, they don't want their old women. These are the kind of people I am talking about. There are so many other ladies who want to dispose their old husbands simply because they are MPs or they are Chairmen of parastatals. This is the kind of thing I am trying to safe-guard. However if somebody surely is divorced I am not on that. Personal social discipline permeating leadership in the society. Widowing is a different issue and I believe about Mandela I have answered to the best of my ability.

Interjection Com.... There is also a fourth one; if a woman leader were to divorce the husband because the husband is

battering her everyday, will you blame her?

Paul Mkulima: (inaudible)-----procedures to take to court because that is allowed in our Constitutional

Com... (Inaudible)----- aman who is battering her everyday and tell her now you cannot hold public office?

Paul Mkulima: Okay, even in mathematic when you are calculating, there are what we call reverse extremes. Those are extremes. Battering a wife running away, you are running for your dear life. That is something else and you can take that person to court. But I was insisting on the social circles, if you have to get into that.

Com. Phoebe Asiyu: But they are also social circle. Let me give you an example: the other day the vice President of Uganda admitted that the husband had been beating her, and the man said only twice, but he had really beaten her bad. Are you telling us that Kazibwe should be sacked from being vice President because she is now divorced?

Paul Mkulima: Alright it is not the vice President that people who was beating the husband. So she has no problem, infact she was getting beaten. So she is not the one who was fighting. She divorced but the divorced did not...

Com. Phoebe Asiyu: She should now leave the vice President,

Interjectin Paul Mkulima: That is what I am trying to answer; the divorce was not caused by her. We have to look at the basis, the root of everything. You see, if it was her who divorced and ran away from the husband, well, then that can be understood. It will fall in this case what I am trying to express.

Com. Phoebe Asiyu: Okay but I thing you also appreciate that we are not making this Katiba for this generation, oh yes it is for this generation, but if it is a good Katiba it should last this country another one hundred years. The American one has lasted over two hundred years and it is still good, it has only been reviewed like fourteen times or may be a litle more than that, but it is still a very steady constitution. I would beg you that you think for the future generations when you make your recommendations.

Paul Mkulima: And I think that is my recommendation. Okay let me touch on the MP becoming the President of the country. If really I am contesting for a parliamentary seat and I have announced that after that, I have an interest to go to the State House, and there is a provision in law which says that the second best candidate will be the MP, and definitely you see the possibility of me going to the State House, then definately you will contest along-side me because you want to be number two. So when you want say the President is never opposed here in Kenya, guys and ladies will start doing so if they see a person has the possibility of going to State House. And I want to say clearly they have been wanting to contest but they have been

harassed to avoid embarrassment to the President. There are so many, you saw what happened to Kandie in Baringo, he was harassed, beaten, he could not sleep at home. Everywhere the police were on his heels, the whole army was taken to his home, he couldn't sleep, the mother, the children, they were all harassed simply because they were opposing Moi and Moi is above the law. That is another point I wish to have mentioned, nobody should be above the law in Kenya because that has been... yes. So what I am trying to say is that these people are barred from contesting and if there is a free atmosphere, you see many people contesting.

Interjection Com... I think we can assume the atmosphere is very free. You are on NPK candidate, you have won the presidency, the second best is a KANU candidate, or SDP, and those people voted for you from your area are actually NPK. So are you being fair for allowing a Member of Parliament from another party?

Paul Mkulima: Okay it is,

Interjection Com... I think that is the question?

Paul mkuilim: Yes it is the people who have got the power to elect, to choose. So it doesn't matter which party, but the second best, whether it is from Shirikisho, Safina, I suggest the second best from any party not necessarily the party which has taken the President to State House. That is what I mean.

Com. Phoebe Asiyo: So you actually deny you President one candidate?

Paul Mkulima: Not really

Com. Phoebe Asiyo: One political...

Paul Mkulima: Not really I am sounding more democratic by taking the second best,

Com. Phoebe Asiyo: Okay, thank you.

Com.. My question there are others okay

Paul Mkulima: Ask me I will try my best I have recorded three questions here which you asked and I have answered. If you ask another one I will go ahead.

Com. Phoebe Asiyo: And you have answered that, because I have been a Member of Parliament for very many years and my

husband was too busy to accompany me to those functions some times he comes sometimes he did come. Are you suggesting I should lose to be a member of parliament because my husbands Mr Asiyo doesnt come with me?

Paul Mkulima: Alright I want to answer that quickly. What we know is that Mrs Asiyo is a stable family woman and we know she has a hold on of her family, and we know she is married. In some occasions, we see your husband with you in state. Some occasions I say. Some occasions. But not all if he is working and engaged in another commitment, or he is leading another, company or something like that. The most important thing is to know that Mrs Phoebe Asiyo is a leader who is leading right from her home, and we know that. Not necessarily, if I may say so. There should be a provision “not necessarily” always, because that will make your husband leave his job to follow you. Any other question?

Com... Yes I have one question. You have talked about the medical examination. What about if somebody is malicious and so decides to falsify the records? Somebody can recommend one is having cancer when you actually don't have. Have you seen the legal cases which are coming up now about even post mortem?

Paul Mkulima: I want to answer that,

Com..... Yes, yes..

Paul Mkulima: We have seen eg pathology report

Com.... No may be the ease is in court, you know once you go for...

Paul Mkulima: Not I am not mentioning names

Com... What we are saying is that have you realized that actually whoever does that medical examination can be malicious?

Paul mkulima: Okay, I wish to say that the test should not be confined to one doctor, because if it is confined to one doctor, then definately he will be manipulated by the ruling party or the people in town.

Com: Before you finish answering that question, you can also have a terminal case like of cancer, even if somebody has cancer it does not mean it wil kill him tomorrow or the next four years, you can go for another twenty years. So why should you deny somebody a chance?

Com. Phoebe Asiyo: And in any case, would it not perhaps become a discrimating policy of denying those who are seffering from an illness but are prepared to still sacrifice for their nation?

Interjection Com: If you go to the International Labour Organization laws they say you can only be retired from your job on medical grounds if because of that disease you can no longer perform. Now if people can still perform, you will be creating another problem in this country of getting people out of employment.

Paul Mkulima: That is where I was coming to. I was saying, any public leader should have medical examination, and if found suffering from a terminal disease which will not, because the medics do understand this which will not and I quote this, 'will not take him for the next four years in Parliament which I am suggesting, then that is the time he should not be allowed. If however it is a slow process thing like cancer which can take him twenty years than I have no objection to that.

Interjection Com. When is this examination taken?

Paul Mkulima: Before and I mean before three months.

Interjection. Com: Before what?

Paul Mkulima: Before elections.

Interjection. Com: Before elections? So are you telling us all people who are aspiring for parliamentary seats must go for medical examination?

Paul Mkulima: That is what I am saying and it is my suggestion. That is what I am saying together with civic, any-body who is going for public office should undergo medical examination and if found to be having terminal disease, he should be disqualified, particularly a terminal disease which cannot last him four years which I am suggesting the parliament should take.

Interjection Com. But let me ask you a question; if somebody is examined and is found to be of sound mind, really what about somebody who is having other diseases in the body which can actually cause termination of, like even malaria is not a terminal disease but it can kill?

Paul Mkulima: But it is treatable. You can treat malaria – you see! I wish to answer any other question you have.

Com. Phoebe Asiyo: You have done very well answering all those questions. Yes Bwana Mkulima. Can we now have... please go and register your name and if you have written anything, it is now our property. Bwana Joseph Katiku, Joseph Katiku please take your seat. We give you five minutes. We want you to give us time for asking you some questions so that we know in details what your recommendations truly are.

Joseph Katiku: Asante sana Mwenyekiti, Commissioner na officials na wananchi. Maoni yangu...

Interjection. Com. Phoebe: Majina yako kwanza.

Joseph Kitiku: Majina yangu ni Joseph Mwithia Mulua Katiku, businessman Matuu. Yangu itakuwa machache sana

Kuhusu political parties, let there as many political parties as needed lakini baada ya election, kutakuwa na ile political party ile itashika usukani, ile itakuwa ruling party, na kutakuwa na ile ingine ambayo itakuwa official opposition party ambayo itakuwa namba mbili ya hiyo. Let other parties be dissolved for that time of parliament ili kuwe na parties mbili.

Ile ingine ni kujiandikisha kuwa candidate katika any political party ama kuenda kwa bunge. Kuwe na wale ambao wanakuwa sponsored by the parties, na kuwe na independent candidates, hata akiwa sio sponsored by any party. Bila ya hiyo nitarudia ile ya kwanza ya kumaliza vile vyama vingine ambavyo havikupata namba mbili ama havikupata official opposition. Wale members wa vile vyama vingine ambavyo vitakuwa dissolved wapewe nafasi ya kuingia either in the ruling party or in the official opposition party.

Interjection Com. Phoebe Asiyu: Those who are elected from other parties

Joseph Kaliku: Those who are elected from other parties wapewe nafasi waingie katika either ruling party or official opposition party.

Political parties viwe vyama vya kushughulikia development ya siasa.

Ile ingine ni kuna Commissions ambazo zimechaguliwa na President wakati ambao anataka kitu fulani kishughulikiwe, kiangaliwe anachagua Commission anasema hawa waangalie kitu fulani. Kama inawezekana, kuwe na independent body ya kuchagua hawa ma-Commissioners, lakini sio President. Kwa upande ya Commissioners nitafika hapo.

Ile ingine ni kwa upande wa corruption, hili neno corruption, imeenda sana hata ikaingia kwa damu, sijui tutatafuta njia gani ya kuiondoa. Nataka kupendekeza kama inawezekana katika kila government office, kuwe na mtu ambaye yuko concerned kwa hiyo office giving any name iwe ya supritendent au what, lakini awe anahusika na yale ambayo yanaendelea kwa hiyo ofisi. Kama ni ku-attend wananchi, unajua wananchi wengine wanatoka hapa katika reserve wanaenda Nairobi, hata pengine hawajafika Nairobi anaonyeshwa ofisi ile ambaye anaenda. Akifika huko ni kuangalia hajui atapita njia gani, hajui ataona nani, hajui ni nani atamshughulikia, na pengine that is where people are ruined. Kwa hivyo kama tutakuwa na huyu mtu ambaye anashughulika juu ya ofisi hiyo, apange mpango, mtu akiingia hata akiwa ni mgeni, hata ikiwa ni kuchukua namba huko achukue

namba na iwe moja tu kwa siku hiyo. Mwishowe aangalie zile namba alipanga asubuhi zote zilikuwa attended, ili kila mtu ashughulikiwe.

Kwa upande wa police, hiyo corruption kwa upande ya polisi, ningeonelea kuwe na kikosi kingine kimoja kinashughulika juu ya corruption. Muweke kikosi kiwe quite independent kisiwe under the Commissioner of the police kiwe independent. Asante sana, maoni yangu itafika hapo.

Com. Pastor Ayonga: Bwana Joseph, umesema hivi vyama kama vile kile kimeshinda ambaye ni ruling party, na kile kingine ambacho kilikaribia opposition party, hivyo viwili viwachwe tu ndiyo, vyama lakini vingine vyote viwe dissolved na parliament?

Joseph Kiliku: Wakati huo

Interjection Com. Pastor Ayonga: Viwe dissolved na parliament wakati huo ili watu hawa wapewe nafasi ya kuingia vyama vingine vyote?

Joseph Kiliku: Hapana vile...

Interjection Com. Waingie kwa ruling.

Joseph Kiliku: Waingie kwa vile vyama viwili vimebaki.

Com. Ruling party.

Joseph Kiliku: Ruling party ama official opposition party.

